

Tafuta rekodi zako za chanjo

Ukipoteza kadi yako ya chanjo unaweza:

- Ulizia kadi mpya pale ulipochanjwa.
- Tafuta rekodi yako mtandanoni katika ‘Sajili ya Chanjo ya (Wisconsin Immunization Registry).’

Sajili ya Chanjo ya Wisconsin (WIR) ni nini?

WIR ni tovuti ambapo unaweza kuona chanjo zote ambazo umepokea mahali popote ndani ya Wisconsin ikiwamo famasia, ofisi ya daktari wako, na kliniki za chanjo.

Unaweza kukosa kuona chanjo ulizopokea zaidi ya miaka 20 iliyopita, hata kama ulizopokea ndani ya Wisconsin.

Je, WIR ni ya faragha?

WIR inafuata sheria zinazolinda taarifa za afya za kibinagsi. Lazima utumie Nambari yako ya Ruzuku ya Serikali, kitambulisho cha Medicaid, au kitambulisho cha Mwanachama wa Huduma za Afya kufikia rekodi zako za chanjo mtandaoni. Hii inakusitiri.

Je, ninaweza kutafuta vipi rekodi zangu za chanjo kwenye WIR?

The screenshot shows a search interface for the Wisconsin Immunization Registry (WIR). The form has fields for First Name and Last Name, Birth Date, and three input boxes for SSN, Medicaid ID, and Health Care Member ID. Below the SSN field is the text "Enter either the Social Security Number, Medicaid ID, or Health Care Member ID:". To the right of the form are three buttons: "Search", "Home", and "Help".

* First Name

* Last Name

* Birth Date

Enter either the Social Security Number, Medicaid ID, or Health Care Member ID:

* SSN

Or

* Medicaid ID

Or

* Health Care Member ID

Search

Home

Help

1. Nenda kwenye: <https://www.dhfsuir.org/PR/clientSearch.do>

Alama ya nyota (*) inaashiria kuwa taarifa hiyo inahitajika.

2. Ingiza:

- jina la kwanza
- jina la mwisho
- Tarehe ya kuzaliwa (MM/DD/YYYY)
- **mojawapo ya haya:**
 - Nambari ya Ruzuku ya Serikali
 - Kitambulisho cha Medicaid
 - Kitambulisho cha Mwanachama wa Huduma ya Afya (uliza nambari hii kwa daktari wako anayekuhudumia kimsingi)

3. Bofya 'tafuta' (search)

4. Tazama orodha ya chanjo zako

5. Bofya 'piga chapa' (print)

Unaweza kuionyesha kazini, shulenii, katika huduma za chekechea, na katika kambi za majira ya joto.

Nitafanya nini ikiwa siwezi kupata rekodi zangu kwenye WIR?

Hakikisha ulijaza taarifa yote sahihi. Ikiwa bado huwezi kupata rekodi zako, tuma barua pepe kwa dhswirhelp@dhs.wisconsin.gov. Kumbuka, unaweza kukosa kuona rekodi zako za kitambo.

Tazama video hii ili kupata maelezo zaidi:

Kiingereza- <https://www.youtube.com/watch?v=BZ2THx6qLcA>

Kihispania- <https://youtu.be/so4cl2cCS9s>

Kiarabu- <https://youtu.be/PLmX0mckJ9M>

Kirohingya- <https://youtu.be/DHIWJKye3iQ>

Kiburma- <https://youtu.be/-w5yttTZ6NM>